## Nina haki zipi kama mgonjwa au mtumizi wa huduma za afya?

**i) Haki ya kupata huduma za afya:** Nina haki ya kupewa huduma za afya zilizo bora na zinazofikika.



**ii) Haki ya afya ya uzazi. Nina haki:**

- Nipewe habari muhimu kuhusu afya ya uzazi;
- Nifikie huduma za afya ya uzazi pamoja na huduma za upangaji uzazi zilizo salama, zinazotenda kikamilifu, zinazokubalika na kwa bei nafuu;
- Nifikie huduma za afya zinazofaa ili niwe salama katika uja uzito, kujifungua, na baada ya kujifungua.
- Nitibiwe na mhudumu aliyepata mafunzo ya taaluma kwa hali zinazonikumba wakati wa ujauzito.



**iii) Haki ya matibabu ya dharura:** Nina haki ya kupata matibabu ya dharura kwa maana ya kuwa wakati wa dharura, kila hospitali, ya umma au ya kibinafsi, inafaa kuhakikisha:

- Nimetunzwa kabla ya kufikishwa hospitali;
- Hali yangu ya afya imethibitiwa; na
- Hospitali imenipangia uhamisho iwapo hawana vifaa au uwezo wa kudhibiti hali yangu ya afya.



**iv) Haki ya kupata habari za afya. Hii inamanisha nina haki ya:**

- kufahamishwa juu ya hali yangu ya afya;
- Kufahamishwa juu ya matibabu ninayopata;
- kujulishwa juu ya faida, hatari, gharama na matokeo ya kila uchunguzi wa matibabu.
- Kukataa mapendekezo ya matibabu niliyopewa(na habari kuhusu matokeo, hatari, na mweleko wa sheria kuhusu kukataa).



**(v) Haki ya kufanya maamuzi kwa kuelewa:**
Kwamba lazima nitoe ruhusa ya kupewa huduma fulani za afya.

**(vi) Haki ya siri:**
Habari kuhusu hali yangu ya afya au matibabu ninayopata katika kituo cha afya zitawekwa siri.

**(viii) Haki ya kuheshimiwa:**
Hadhi yangu lazima iheshimiwe na kulindwa wakati ninapopata huduma za afya.

**(ix) Haki ya kutobaguliwa:**
Nina haki ya kupata huduma za afya bila ya kubaguliwa kwa sababu zozote zile. Kwa mfano, iwapo mimi ni shoga, nina haki ya kupewa huduma za afya bila ya kujali mwelekeo wangu wa kijinsia.

**(x) Watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano wana haki ya kupata chanjo za lazima bila malipo.**
**(xi) Serikali za kaunti na kitaifa lazima zitoe huduma za afya ya uzazi za msingi bila malipo.**


**Wasiliana nasi:**

Ofisi ya Nairobi
Kuwinda Lane, off Lang'ata Road, Karen C
112 - 00202 Nairobi
+254 710 261 408
+254 788 220 300
info@kelinkenya.org
www.kelinkenya.org
@KELINKenya

Ofisi ya Kisumu
Nyalenda Railways Estate Block 9/220
+254 (57) 253 2664
+254 708 342 197
info@kelinkenya.org
www.kelinkenya.org
Facebook/kelinkenya


KELIN Reclaiming Rights, Rebuilding Lives — amkeni waKENYA — UNDP

# Tambua Haki Zako; Haki ya Afya



## Je nina haki ya afya?

NDIO. Kitengo cha 43 (1) (a) cha katiba kinamhakikishia kila Mkenya haki ya kupata kiwango cha juu zaidi cha afya, pamoja na haki ya kupata huduma za afya, pamoja na huduma za afya ya uzazi.

## Inamaanisha nini kupata haki ya afya?

- Haki ya mfumo unaotoa nafasi sawa kwa kila mtu kupata kiwango cha juu zaidi cha huduma za afya;
- Kwamba hospitali, kliniki, madawa, na huduma zitolewazo na wafanya kazi wa afya zitakuwa na ubora na zinazokubalika, zitapatikana, zitafikika na kila mmoja;
- Utapata haki ya kuzuia, kutibiwa na kuthibiti magonjwa
- Utakuwa na haki ya kupata madawa muhimu
- Utapata huduma za afya ya mama, afya ya watoto na afya ya uzazi
- Utapata usawa na kufikia huduma za afya za msingi kwa wakati ufaao
- Utapata maelezo na habari zinazohusiana na maswala ya afya
- Utashirikishwa katika kufanya maamuzi yanayohusiana na maswala ya afya katika viwango vya kitaifa na kijamii.

## Ni nani atahakikisha ninatimiziwa haki yangu ya af ya?

Ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa ninatimiziwa haki yangu ya afya.

Chini ya kitengo 21(1) cha Katiba ya Kenya, serikali ina jukumu la kutekeleza, kuheshimu, kulinda, kuendeleza na kutimiza haki na mapendeleo ya msingi, ikiwa ni pamoja na haki ya afya.

- **Jukumu la kuheshimu** linamaanisha kuwa serikali haitatiza kutimizwa kwa haki yangu ya afya.
- **Jukumu la kulinda lina** maana ya kwamba itachukua hatua kuwazuia watu wasiohusika kutatiza kutekelezwa kwa haki yangu ya afya.
- **Jukumu la kuendeleza** linamaanisha kuwa serikali itakuwa na mikakati ya kuhamasisha watu kuelewa na kuheshimu haki ya afya.
- **Jukumu la kutimiza** lina maana kwamba serikali itakuwa na mikakati ya kisheria, kiutawala, kiuchumi, mahakama, uhamasishaji na mingine kuhakikisha haki ya afya imetekelezwa.

### Kwa hivyo, kati ya mengineyo serikali ina jukumu la:

- Kuhakikisha kuwepo na utaratibu wa utoaji huduma za afya katika viwango vyote vya mfumo wa afya;
- Kukuza sera, sheria na mipango mingine muhimu katika kulinda, kuendeleza, kuboresha na kukimu afya na ubora wa maisha ya kila mmoja;
- Kuhakikisha kutangulizwa na kuwekeza kwa ajili ya utafiti kuhusu afya;
- Kuhakikisha utekelezwaji wa haki nyingine zinazohusiana na afya na mahitaji ya watu wanaoishi katika hali ngumu katika jamii, hii ikiwa ni pamoja na wanawake, wakongwe, walemavu, watoto wadogo, vijana, makabila madogo au waliotengwa au watu wa kabila, dini, au tamaduni fulani.

## Serikali inapaswa kukujulisha mambo yapi kuhusiana na afya?

Ili nipate haki yangu ya afya, serikali ya kaunti au kitaifa inafaa kunipa habari zifuatazo:

- Aina za huduma za afya, upatikanaji na gharama yake
- Mipangilio na utaratibu wa utoaji wa huduma za afya
- Masaa ya kazi na ratiba ya wahudumu wa afya kutembelea vituo vya afya
- Taratibu za kufikia huduma za afya
- Taratibu za kutoa malalamishi
- Haki na majukumu ya watumizi na watoaji huduma za afya
- Usimamizi wa shughuli za kulinda mazingira na kumaliza hatari zinazokabili afya ya jamii

*Imeasiliwa kutoka tovuti ya Mwongozo wa Afya na Haki za Binadamu*

## Vidhihirisho vya msingi vya haki ya afya

Kuna maswala ya kijamii na kiuchumi yanayochangia vile watu wanavyoendeleza maisha ya afya. Haya ni pamoja na:




Ufikiaji wa mafunzo na habari kuhusiana na afya



Upatikanaji wa chakula cha kutosha kilicho salama



Kupata makazi



Kupata mazingira safi



Maji ya kunywa yaliyo salama



Lishe bora toshelevu



Mazingira ya kufanya kazi yanayoendeleza afya

*Imeasiliwa kutoka kwa Shirika la Afya Duniani (WHO) (2009). Geneva: WHO.*

# Vipengele muhimu kwa haki ya afya

Huduma zote, bidhaa na vifaa lazima vipatikane, vifikiwe, vikubaliwe na viwe bo ra.

### Upatikanaji:

Vifaa vya afya ya umma na huduma za afya, bidhaa na huduma lazima vipatikane na viwe vya kutosha. Vifaa hivi ni pamoja na:
(i) vigezo vya msingi vya afya pamoja na maji safi na vifaa vya usafi wa mazingira;
(ii) hospitali, kliniki au majengo mengine ya utoaji wa huduma za afya;
(iii) wahudumu wa afya na wafanyakazi waliopata mafunzo rasmi, na
(iv) madawa muhimu.

### Ufikikaji:

- Kutobaguliwa: vifaa vya afya, bidhaa na huduma lazima zifikiwe na watu wote, hasa makundi ya watu waliotengwa na wanaoishi katika hali ngumu.
- Miundo msingi inayofikika: vifaa vya afya, bidhaa na huduma, matibabu, na mahitaji ya msingi ya afya yatolewe katika mazingira salama yanayofikika na kila sehemu ya umma.
- Kufikiwa kiuchumi (uwezo wa kumudu kulipa): vifaa vya afya, bidhaa na huduma ziweze kugharimiwa na watu wote.
- Kufikiwa na habari: habari lazima zifikiwe- hii ni pamoja na haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza habari na maoni juu ya afya, huku tukiheshimu haki ya kuziweka siri habari za afya za mtu binafsi.

### Kukuba lika:

Vifaa, bidhaa na huduma viheshimu maadili ya matibabu, viheshimu tofauti za jinsia na kukubalika kimila. Lazima zikubalike kimatibabu na kimila.

### Ubora:

- Vifaa, bidhaa na huduma ziwe bora zinazofaa kisayansi na kimatibabu.
- Lazima kuwe na wahudumu wa afya waliopata mafunzo ya taaluma, madawa yaliyokubalika kisayansi yasiokaa muda mrefu, vifaa vya hospitali, vifaa na miundo ya usafi na maji ya kunywa yakiyosalama.

*Imeasiliwa kutoka tovuti ya Mwongozo wa Afya na Haki za Binadamu*